BRITISH COUNCIL #EastAfricaArts

*new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)* **(nAnA) ya mwaka 2018**

**Kitini cha Maelezo kwa ajili ya mwombaji**

YALIYOMO:


Ukurasa 2 | nAnA ya mwaka 2018 Maelezo Muhimu na Sifa

Ukurasa 3 | Vigezo, Mchakato na Ratiba

Ukurasa 4 – 6 | Maswali yanayoulizwa Mara kwa Mara

## new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) (nAnA) kwa mwaka 2018

*new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) (nAnA)* ni mwito unaotolewa kila mwaka kwa: wasanii wenye umri kati ya miaka 18 na 35, mashirika yanayojishughulisha na sanaa, na vikundi vya wasanii kutoka miji ya Wingereza, Ethiopia, Kenya; Ireland ya Kaskazini; Rwanda; Scotland; Sudan ya Kusini; Sudan; Tanzania; Uganda; na Wales. nAnA inawapa wasanii fursa kutoka nchi hizi ili waweze kubuni sanaa mpya kwa kushirikiana kwa pamoja na kufanya maonyesho ya sanaa hizo kwa hadhira inayotoka katika nchi hizi.

## Maelezo Muhimu ya nAnA kwa mwaka 2018:

1. nAnA itafadhili miradi mipya 5 kwa mwaka 2018;
2. Kiasi kisichozidi £30,000 kitatengwa kwa ajili ya kila mradi;
3. Wasanii, mashirika yanayojishughulisha na sanaa na/vikundi vya wasanii kutoka nchi maalum **(zilizotajwa hapo juu)** watatakiwa waungane ili washirikiane kutengeneza, kuwezesha, au kutayarisha kwa pamoja sanaa mpya. Mifano inayo onyesha namna mbalimbali ya kutafsiri kigezo hiki inapatikana katika sehemu inayohusu Maswali yanayoulizwa mara kwa mara katika ukurasa wa 4;
4. nAnA ya mwaka 2018 inalenga hasa kusaidia miradi ya wasanii, mashirika yanayojishughulisha na sanaa na/vikundi vya wasanii ambavyo tayari vinashirikiana na wenzao wa nchi jirani au vile ambavyo vinataka kukuza ushirikiano na mahusiano na wasanii wengine. Vilevile vikundi vitasaidiwa katika kutafuta washirika wapya, na katika maelezo kuhusu maswali yanayoulizwa mara kwa mara, utapata kuona namna ambavyo British Council inasaidia wasanii kupata washirika kutoka Wingereza na Afrika Mashariki;
5. Sanaa na mada za aina zote zinakaribishwa

## nAnA ya mwaka 2018 Sifa za Mwombaji/Waombaji:

1. Maombi yanaweza kutumwa na msanii mmoja au zaidi, shirika moja au zaidi linalojishughulisha na sanaa, au kikundi cha sanaa kimoja au zaidi;
2. Kila mradi utatakiwa ujikite zaidi katika utengenezaji wa kipande kipya au kazi mpya ya sanaa;
3. Mradi unaopendekezwa ni lazima uhusishe walau nchi **tatu** ambazo **mbili** kati yao ziwe ni za Afrika Mashariki (na ziwe kati ya zile zilizotajwa hapo juu);
4. nAnA imejikita katika kusaidia sekta za sanaa za **mijini** kutoka nchi zilizotajwa hapo juu– wasanii, kazi za sanaa, na hadhira wawe na uhusiano na miji;
5. Kila mradi unatakiwa uwe umelenga kuwafikia moja kwa moja watu wenye umri kati ya mika 18 na 35, na hadhira inayoshiriki kwa njia ya mtandao wa intaneti. Dhumuni la nAnA ni kuongeza mwonekano na ufahamu wa sanaa za leo kutoka Afrika Mashariki na Wingereza. Hivyo, suala la kuifikia hadhira moja kwa moja au kwa kupitia mtandao wa intaneti ni muhimu;
6. Wachangiaji wakuu wanaohusika na mradi wanatakiwa wawe na umri kati ya miaka 18 na 35;
7. Miradi hii inaweza kuchangiwa, sehemu ya gharama, na zaidi ya mfadhili mmoja;
8. Mwombaji anaweza kutuma zaidi ya ombi moja kwenda kwa new *Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya);*
9. Mwombaji aliyepata fedha za nAnA 2016/17 (haijalishi kama alishiriki kama mfadhiliwa mkuu au mdogo) anaweza kuomba fedha za nAnA 2018. Hata hivyo, mfadhiliwa aliyeshiriki kama mshirika mkuu wa nAnA 2016/17 **hatoweza** kufadhiliwa kama mshirika mkuu wa nAnA 2018;

10. Miradi yote itatakiwa itekelezwe na ikamilike ndani ya kipindi cha miezi 12 baada ya kupokea fedha kutoka British Council;
11. Ili fedha zihidhinishwe ni lazima iandaliwe ripoti ya utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha nusu mwaka na ya mwisho wa utekelezaji. Mfumo wa uandishi wa ripoti hizi utawekwa bayana;
12. Mradi utatakiwa usimamiwe na mtu mmoja au shirika moja. Lazima wawe na akaunti ya benki na kitambulisho cha Taifa iliwaweze kupokea fedha. Vilevile watakuw na jukumu la kusimamia ripoti ya mradi ya nusu mwaka na ya mwisho wa mradi, pamoja na mawasiliano kwa umma kuhusu mradi.
13. Asilimia 70 ya fedha itatolewa mara baada ya mkataba kutiwa saini na British Council, asilimia 30 iliyobaki itatolewa mara baada ya kuwasilisha ripoti ya mradi ya kipindi cha nusu mwaka.

**Tizama katika kiunganishi hiki iliupate habari juu ya miradi ya nAnA ya mwaka 2016/17:**
https://www.britishcouncil.org/east-africa-arts/projects/nana

## Vigezo vitakavyozingatiwa kwa waombaji wa nAnA kwa mwaka 2018:

Baada ya mchujo wa barua za maombi na uandaaji wa orodha ya watakaofanyiwa usaili, jopo la usaili litakalofuata litauliza maswali 5 ya fuatayo:

1. Je, mradi huu unapendekeza utayarishaji wa **sanaa mpya** ya leo yenye ubunifu?
2. Je, sanaa hii mpya iatatengenezwa na / maonyesho yake kufanyika kwa kupitia **ushirikiano imara** kati ya wasanii, mashirika yanayojishughulisha na sanaa na / au vikundi vya wasanii katika nchi zilizotajwa?
3. Sanaa hii mpya itaifikiaje **hadhira mpya** ambayo inashiriki kwa njia ya mtandao wa intaneti na nyingine inayoshiriki moja kwa moja katika nchi za Wingereza na za Afrika Mashariki? Hadhira itakayofikiwa inaukubwa gani? Nini makadirio ( kwa tarakimu) ya idadi ya hadhira inayotegemewa kufikiwa na je, tarakimu hizi ni halisi?
4. Wachangiaji wakuu (wasimamizi, watayarishaji, wasanii, waratibu, na waombaji) katika mradi huu, je ni watu wenye umri kati ya miaka 18 na 35? Na hadhira ya mradi huu, je wengi wao ni watu wenye umri kati ya **miaka 18 na 35?**
5. Je **bajeti** ya mradi huu umechanganuliwa na kufanyiwa utafiti wa kutosha na je ni halisia?

## Mchakato wa uchaguzi wa nAnA wa mwaka 2018:

Iliuweze kutuma ombi lako kwenda kwa *new Art new Audiences* (*Sanaa Mpya Hadhira Mpya)* utatakiwa ukamilishe maombi yako kwakupitia fomu ya maombi kwa njia ya mtandao wa intaneti ambayo inapatikana hapa: https://www.britishcouncil.org/east-africa-arts/opportunities

Maombi yanayofanywa kwa njia ya mtandao wa intaneti yatahusisha **maswali 5** yanayolenga kuchambua wazo la mradi wako: ushirika na ushirikiano na nchi, miji (iliyotajwa hapo juu) pamoja na washirika wako uliopanga kujenga; ufikiaji wa hadhira; ratiba na mpango wako wa mawasiliano; na bajeti yako. Pia utapata fursa ya kuambatanisha picha au video na nyenzo nyingine ambazo utapenda kuzitumia.

Mara baada ya kutuma ombi lako utapata barua pepe ikikufahamisha kuwa ombi lako limepokelewa. Utafahamishwa siku ya Jumatatu, 13 August kama mradi wako umepita katika orodha yawatakaofanyiwa usaili. **Angalizo: hutofahamishwa chochote kama mradi wako haukupita katika**

**orodha ya watakaofanyiwa usaili.** Zoezi la usaili litaendeshwa na mameneja wa sanaa wa British Council katika kila nchi ambako nAnA unatoa ufadhili.

Iwapo utakua umefanikiwa kupita katika orodha ya watakaofanyiwa usaili, utaitwa katika usaili utakao fanyika kwa njia ya Skype na zoezi litadumu kwa muda wa **dakika 45 hadi saa 1.** Utatakiwa uwasilishe yaliyomo ndani ya barua yako ya maombi kwa kuzingatia maswali 5 yaliyotajwa hapo juu.

Waombaji wote waliofanyiwa usaili lakini hawakufanikiwa kupita watapatiwa majibu yao kama watayaomba.

### Ratiba ya mchakato wa uchaguzi wa nAnA kwa mwaka 2018:

- Maombi ya ufadhili yanakaribishwa kuanzia **Jumatatu, 4 Juni;**
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **Jumapili, 15 Julai, saa 6 usiku saa za Wingereza;**
- Mchujo wa kupata orodha ya watakaofanyiwa usaili utafanyika: **Jumatatu, 16 Agosti – Jumapili, 12 Agosti** ;
- Waombaji waliochaguliwa kufanyiwa usaili watafahamishwa na kuitwa katika usaili: **Jumatau, 13 Agosti;**
- Usaili kwa njia ya Skype utafanyika kwa wale waombaji waliochaguliwa kufanyiwa usaili: **Jumatatu, 27 Agosti – Ijumaa, 31 Agosti ;**
- Mchujo wa mwisho: **Ijumaa, 14 Septemba;**
- Waombaji wote kufahamishwa matokeo ya usaili: **Jumatatu, 17 Septemba;**
- Malipo kwa miradi: **Septemba/Octoba 2018;**
- Tarehe ya Miradi kuanza: **1 Novemba 2018.**

## *new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) (nAnA) | Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Toleo hili limeboreshwa mara ya mwisho: 8 Mai 2018

**Je kama sifahamu washirika wangu ni nani katika hatua hii?**

Kabla ya kutuma pendekezo lako la *new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)*, tunategemea kuwa waombaji watakuwa wameshafanya uchunguzi na kuchagua washirika watakaofanya nao kazi katika nchi zilizotajwa. Malengo ya Programu ya Sanaa ya British Council katika Afrika Mashariki ni kujenga uhusiano baina ya wasanii watayarishaji wenye umri kati ya miaka 18 na 35 kutoka Afrika Mashariki. Ilikukusaidia kutafutaj watayarishaji na washirika utakaofanya nao kazi, tunapenda kuwapatia tovuti za British Council zifuatazo ambazo zinaainisha wasanii watayarishaji wanaotekeleza miradi inayosisimua Afrika Mashariki na Wingereza.

***Afrika Mashariki na Wingereza:***

Tovuti ndogo ya Sanaa za Afrika Mashariki: www.britishcouncil.org/east-africa-arts

Sanaa za Afrika Mashariki za ukurasa wa Instagram: www.instagram.com/eastafricaarts

***Aina za Sanaa za Wingereza:***

Sanaa za Uoneshi: http://visualarts.britishcouncil.org

Usanifu, Ubunifu na Mitindo: http://design.britishcouncil.org

Fasihi: https://literature.britishcouncil.org

Maigizo na Dansi: https://theatreanddance.britishcouncil.org

Muziki: http://music.britishcouncil.org

Filamu: http://film.britishcouncil.org

***Aina za Sanaa:***

Sanaa na Utamaduni wa kidijitali: https://medium.com/intersections-arts-and-digital-culture-in-the-uk

Uchumi wa Sanaa: http://creativeconomy.britishcouncil.org

Stadi za kitamaduni: https://www.britishcouncil.org/cultural-skills-unit

Utamaduni na Maendeleo: https://www.britishcouncil.org/arts/culture-development

Kitovu cha ubunifu: http://creativeconomy.britishcouncil.org/projects/hubs/

Ukurasa wa Nyumbani wa Sanaa za British Council: https://www.britishcouncil.org/arts

**Angalizo: Ilikuhakikisha kuwa waombaji wote wanapatiwa habari sawa, British Council haitoweza kuwaunganisha moja kwa moja waombaji na washirika katika kipindi hiki au kwa ajili ya mwaliko huu wa *new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)*.**

**Kwanini ni lazima niwe na umri kati ya miaka 18 na 35?**

Programu ya Sanaa ya British Council katika Afrika Mashariki inatoa kipaumbele kwa suala la kuwaunganisha vijana wabunifu kati ya Wingereza na Afrika Mashariki kulingana na mkakati wake katika ngazi ya kanda: http://bit.ly/2gV6rFz Tunafahamu kuwa mara nyingi hii sio rahisi, hivyo tunashauri kuwa waombaji, washiriki, na hadhira ya mradi, kwa kadri iwezekanavyo, wawe wa umri kati ya miaka 18 na 35.

Zipo fursa nyingi za kimataifa ndani ya British Council ambazo unaweza kuziomba, tizama hapa: https://www.britishcouncil.org/arts/opportunities

**Ni kipi hakifadhiliwa na *New Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)*?**

- Warsha, Mikutano na Kongamano – isipokuwa tu pale ambapo kutakuwepo na uhusiano wa moja kwa moja na uundwaji wa sanaa mpya;
- Sanaa ambayo tayari ilikwishatengenezwa kabla ya kupata ufadhili wa *new Art new Audiences*;
- Miradi ambayo hailengi kufikia hadhira mpya.

**Nini maana ya *Sanaa Mpya*?**

British Council inafanyakazi na aina nane za sanaa. Nazo ni Usanifu, Mitindo, Filamu, Dansi na Maigizo; Uchumi wakibunifu; Stadi za Kitamaduni; Fasihi; na Sanaa za Uoneshi.

*new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)* inatafuta miradi itakayotengeneza sanaa mpya kwa kutumia aina ya sanaa moja wapo au kwakuzingatia zaidi ya aina moja. Aidha, tanatafuta miradi inayo hoji aina hizi za sanaa. Ambacho hatutaki ni zile kazi za sanaa ambazo tayari zimeshatengenezwa.

**Ni nchi zipi zinahusika katika mwito huu wa *new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)?**

Katika mwaka 2018 Programu ya Sanaa ya British Council Afrika Mashariki pamoja na mfuko wa *new Art new Audiences (Sanaa Mpya Hadhira Mpya)* inafanyakazi katika nchi zifuatazo: Wingereza; Ethiopia; Kenya; Ireland ya Kaskazini; Rwanda; Scotland; Sudan ya Kusini; Sudan; Tanzania; Uganda; na Wales. Tunafanya kazi katika zile nchi ambako zipo ofisi za British Council pamoja na rasilimali zake.

**Je, mwombaji ni lazima awe raia au mkazi wa nchi zilizotajwa ili aweze kutuma maombi?**

**Waombaji** wa mfuko wa *new Art new Audiences* wanatakiwa wawe raia wa Wingereza; Ethiopia; Kenya; Ireland ya Kaskazini; Rwanda; Scotland; Sudan ya Kusini; Sudan; Tanzania; Uganda; na Wales. Waombaji wanatakiwa wawe na vibali vya kuishi au kufanya kazi katika nchi hizi. **Washiriki** wa mradi wanatakiwa wawe raia wa nchi hizi. **Hadhira** inayoshiriki katika mradi nao wengi wao wanatakiwa wawe raia wa nchi hizi lakini wanaweza kutoka nchi nyingine yeyote.

**Nini Maana ya Hadhira Mpya?**

*new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) inalenga kuwa chachu kwa hadhira kutoka Wingereza iliiweze kuona sanaa mpya kutoka kwa wanaAfrika Mashariki, na hadhira ya Afrika Mashariki kuona sanaa mpya kutoka kwa Waingereza. *new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) inalenga ile miradi itakayo fanya maonyesho ya sanaa kwa hadhira ambayo wengi wao wana umri wa kati ya miaka 18 na 35 na ambao hawajawahi kuona sanaa yako. Hadhira ambayo ipo siku zote nayo inakaribishwa, lakini pendekezo lako la *new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) linatakiwa lionyeshe namna ambavyo mradi wako utaifikia hadhira mpya kwa ajili ya sanaa yako.

**Je, ninaweza kutuma maombi kama mtu binafsi?**

Kama unayo akaunti ya benki, kitambulisho cha taifa, na unaweza kuthibitisha uwezo wako wakusimamia miradi mikubwa, *new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) iko tayari kupokea maombi kutoka kwa watu binafsi. Walau nchi **tatu** zihusike katika mradi na **mbili** kati yao ziwe nchi za Afrika Mashariki (na hasa zile nchi zilizotajwa katika kitini hiki cha mwombaji).

**Mradi wangu unatakiwa uanze lini?**

Miradi yote inayofadhiliwa na *new Art new Audiences* (Sanaa Mpya Hadhira Mpya) inatakiwa ikamilike ndani ya miezi 12 mara baada ya kupokea fedha.

**Unamaanisha nini ukisema: "Wasanii, Mashirika yanayojishughulisha na Sanaa na / vikundi vya sanaa ni lazima vishirikiane kutengeneza, kuwezesha, au kuzalisha kazi mpya ya sanaa"?**

Zipo nyingi ambavyo tunaweza kushirikiana katika utayarishaji wa kazi mpya za sanaa. Hapa chini utapata baadhi ya mifano inayoonyesha namna ambavyo ushirikiano huu unaweza kufanyika:

- **Kikundi cha Sanaa cha Rwanda** kitatengeneza kazi mpya ya dansi **na wasanii wa sanaa za maonyesho** kutoka **Kenya** na maonyesho ya kazi hii yanaweza kufanyika katika tamasha nchini **Scotland** kwa kusadiwa na **Mtayarishaji wa Kazi za Kitamaduni** kutoka Scotland;
- Msanii wa kidijitali kutoka **Scotland** atatengeneza kazi mpya ya sanaa kwa kushirikiana na wasanii kutoka **Wales**, **Uganda**, na **Tanzania**. Maonyesho ya kazi hii yanafanywa mtandaoni kwa hadhira ya watu wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35 walioko **Wingereza** na **Afrika Mashariki wakiwezeshwa na gazeti la kidijitalila la sanaa la Afrika Mashariki**;
- **Fundi sauti** kutoka **Sudan** anafanya kazi na wasanii kutoka **Ireland ya Kaskazini** na **Kenya** ilikuzalisha kazi mpya ya sanaa ambayo itaonyeshwa katika tamasha la simu za mikononi katika nchi za **Uganda** na **Sudan ya Kusini**;
- **Shirika linalojishughulisha na sanaa** kutoka **Wingereza** litafanyakazi na **wapiga picha** kutoka **Ethiopia** na **Uganda** ilikuzalisha kazi mpya ya sanaa ambayo maonyesho yake yatafanyika katika onyesho la kimataifa nchini **Tanzania**.